

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

NCHI ZA AFRIKA ZATAKIWA KUWA NA UCHUMI HURU USIOTEGEMEA MATAIFA YALIYOENDELEA.

Nchi za Afrika zimetakiwa kuwa na uchumi huru usiotegemea mataifa yaliendelea ili kuepuka kuathirika na kuyumba kwa uchumi wa mataifa makubwa.

Mkurugenzi wa masuala ya maendeleo ya uchumi kutoka Ushirikiano wa maendeleo ya Afrika (NEPAD) Profesa Emmanuel Nnadozie alitoa kauli hiyo jana mjini Abidjan wakati wa mkutano na waandishi wa habari juu ya funzo ambalo Afrika imelipata kutokana na mtikisiko wa uchumi duniani.

Alisema kuwa hatua hiyo inawezekana iwapo nchi za Afrika zitaimarisha uchumi shirikishi usiotegemea nchi zao kuingiza fedha za kigeni. Profesa Nnadozie aliongeza kuwa nchi za Afrika zinapaswa kuongeza ukuaji na ukusanyaji wa mapato ya ndani kama nchi zingine zinazo jitegemea.

Aidha alisisitiza kuwa Serikali za Afrika zinapaswa kuunga mkono kwa dhati juhudi za sekta binafsi ili

ziweze kuchangia kikamilifu katika ukuaji wa uchumi na kuongeza ajira kwa wananchi wengi barani humo.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa hatua hiyo itasaidia kuwepo na mabadiliko ya haraka na chanya kwa nchi za Kiafrika hali itakayowafanya kuonekana uchumi wao kuwa unazidi kuimarika.

Naye Mchumi na mtafiti kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) Peter Walkenhorst alisema kuwa, Serikali za Kiafrika zinapaswa kushirikiana na sekta binafsi kuongeza nguvu katika uimarisha miundo mbinu kama hatua ya kuimarisha uchumi wao wa ndani.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuwekeza zaidi katika miundombinu mbalimbali kama vile barabara, reli, usafiri wa majini na wa angani.

Aliongeza kuwa kutokana na ushirikishwaji wa sekta binafsi sekta ya mawasiliano ya simu imefanikiwa kupanua kwa kasi kuliko sekta nyingine ambazo bado zinategemea nguvu za serikali ili kuimarishwa.

Katika hatua nyingine Rais wa Ivory Coast Laurent Gbagbo anatarajia kufungua Mkutano wa 45 wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) Alhamis wiki hii, mkutano huo unawajumuisha wajumbe mbalimbali duniani na Tanzania ikiwa ni mojawapo.

IMETOLEWA NA MSEMAJI MKUU

WAZARA YA FEDHA NA UCHUMI

ABIDJAN

24.05.2010